OFISI YA RAIS-TAMISEM
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI ILAMBILOLE,
S.L.P 1439,
IRINGA,
13- 12- 2020,
SIMU: 0765398616.

KUMB:NA.IDC/DEO/ILBSS/JF

JINA LAMWANAFUNZI ……..
S.L.P ……
IRINGA.

YAH : MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILAMBILOLE ILIYOPO WILAYA YA IRINGA (V) MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ilambilole mwaka 2021. Shule hii ipo umbali wa km 35 kutoka Iringa mjini kupitia barabara ya Dodoma. Usafiri unapatikana stendi kuu ya zamani ya Mkoa wa Iringa kwa mabasi yaendayo Ilambilole moja kwa moja.Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11-01-2021,hivyo: unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11-01-2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 19-01-2021 ndani ya siku saba.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 Sare za shule.

(a) Wavulana: Shati mbili nyeupe tetroni mikono mirefu,suruali mbili rangi kijivu namba moja ya kuiva, suruali iwe na serebration (linda) na ikunjwe chini (turn up).

(b) Wasichana: shati mbili nyeupe tetroni mikono mirefu,sketi mbili rangi kijivu namba moja ya kuiva ziwe na linda box.

(c) Rangi ya hijabu ni **nyeupe**.

(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni Track-suti nyeusi kwa wavulana na wasichana.

(e) Raba za michezo rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana.

(f) Bukta nyeusi za michezo kwa wavulana.

(g) T.shirt (singland) nyeupe ya kuvalia shati ya shule kwa wavulana na shumizi nyeupe kwa wasichana.

(h) Viatu vyeusi vya ngozi viwe na kamba –jozi mbili.

(i) Soksi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana-jozi mbili.

(j) Sweta rangi ya damu ya mzee.

(k) Shamba dress (nguo za kushindia).Wavulana-suruali nyeusi ya kitambaa na T-shirt ya blue isiyo na maandishi. Wasichana: gauni kitambaa draft nyeupe (kimeambatanishwa kwenye fomu hii

2.2 Maagizo mengine muhimu.

(a) Fagio (chelewa).
(b) Faili moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake.
(c) Daftari kumi (10) counter book quare 3 au 4
(d) Peni, kalamu na mkebe wa hesabu.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria hizi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivoboreshwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji na usimamizi wa Elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia haya:

(a) Kuheshimu bendera ya Taifa
(b) Kuheshimu viongozi,walimu,wazazi,wanafunzi wenzako na jamii yote kwa ujumla
(c) Kuhudhuria vipindi vyote darasani na shughuli zote ndani na nje ya shule ni ni lazima.
(d) Kuhudhuria vipindi vya jioni (preparation) na vipindi vya dini kila siku kabla ya vipindi vya kujisomea jioni (prepo) ni lazima.
(e) Kuwahi kufika shuleni kila siku kulingana na ratiba ya shule.
(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuizingatia kikamilifu.
(g) Usafi wa mwili,mavazi na mazingira ni muhimu kila siku.
(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(j) Kutunza mali ya umma.
(k) Katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanakuwa na nidhamu nzuri itakayo wapelekea wafanye vizuri kitaaluma, shule hii inajali sana ibada kwa kulingana na imani ya mwanafunzi husika, hivyo hapa shuleni ibada ni lazima kwa waisilamu (ijumaa), sabato (jumamosi) na wakristo wengine jumapili. n.k

4.0 **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile,uvutaji bangi, cocaine,mirungi,kubeli, kucheza kamali n.k.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi
(g) Kudharau bendera ya Taifaa
(h) Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma,kuchochea au kuongoza mgomo,kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa au kumiliki simu

5.0 **MAMBO MUHIMU UNAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHA SHULENI**.

(i) Form ya hospital (medical examination) iambatanishwe na form hii ikiwa imejazwa na daktari wa hospitali ya serikali. *Tafadhali,mwanafunzi apimwe na fomu hiyo igongwe muhuri*.
(ii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelekezo Mengine yatakayotolewa na shule.
(iii) Form ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo namakosa ya jinai.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKINOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI ILAMBILOLE
FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

- JINA KAMILI ……
- Mahali ulipozaliwa ……
- Tarehe ya kuzaliwa ……
- Anuani ya nyumbani ……
- Jina la mzazi /mlezi ……Namba yake ya simu ……
- Anuani ya mzazi /mlezi (kama ni tofauti na hiyo hapo juu) ……
- kazi ya mzazi/mlezi ……
- **Ndugu wa karibu**,

JINA	UHUSIANO	ANUANI YAKE	SIMU
…….	……	……..	…….
……..	……	……	…….
……..	……..	……..	…….

- ✓ Dini ……..
- ✓ Kidato ulichopokelewa ……..
- ✓ Shule uliyomaliza darasa la saba ……
- ✓ Namba yako ya mtihani wa darasa la saba ……..
- ✓ Michezo unayoipenda mbali na masomo ……..
- ✓ Wilaya unakotoka …… Mtaa/kijiji …….kata ……
- ✓ Saini ya mwanafunzi …… Tarehe ……
- ✓ Saini ya mzazi/mlezi ……Tarehe ……

MEDICAL EXAMINATION FORM

ILAMBILOLE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 1436, IRINGA –TANZANIA

TO BE COMPLETED BY: Medical officer in respect of all FORM ONE entrants

Full name ……..
Age ……..
Blood count (red and white) ……..
Stool Examination …….
Urine Analysis (pregnant. YES/NO 0nly for girls)……
Syphilis Test …….
Eye Test ……
T.B Test …….
Ears ……
Chest ……..
Spleen ……..
Abdomen ……..

ADDITIONAL INFORMATION.

E.g. Physical or chronically family diseases, etc

……
……
……

I certify that, the above named student is fit/not fit to pursue studies,

Signature ……..
Designation …….
Section ……
Date ……

STUDENTS:
You must bring this complete filled form when you come to school. No student may be enrolled without certificate of physical fitness.

……..
ALDA J MYENZI
MKUU WASHULE